KATIKA MAHKAMA KUU YA ZANZIBAR

IMESIKILIZWA TUNGUU

RUFAA YA MADAI NAM. 52 YA 2021

(KUTOKA RUFAA YA MADAI NAM. 42 YA 2020 (KADHI WA RUFAA) NA KESI YA MADAI NAM. 355 YA 2020 (KADHI WA WILAYA MWANAKWEREKWE))

TAUHIDA RAMADHAN ABDALLA … … MKATA RUFAA

VERSUS

ALI ALI ALI … … MPINGA RUFAA

HUKUMU

TAREHE YA UAMUZI: 21.7.2022

MBELE YA: MHESH. ISSA, A. A., J

SHEIKH SAMEER ZULFIKAR

SHEIKH SALEH HAKIM

SHEIKH JUMA FAKIH

SHEIKH KANI MKANGA

Hukumu hii inahusiana na rufaa iliyowasilishwa Mahakamani na kupewa namba 52 ya mwaka 2021. Rufaa hii iliwasilishwa na Tauhida Ramadhan Abdalla dhidi ya Ali Ali Ali Rufaa hii inapinga uamuzi uliotolewa na Kadhi wa Rufaa Sk. Daud Khamis Salum.

Kwa ufupi rufaa hii inatokana na Kesi ya Madai Nam. 355 ya 2020 iliyoanzia katika Mahakama ya Kadhi wa Wilaya Mwanakwerekwe ambayo ilisikilizwa na Sk. Othman Ame Chum. Mdai katika kesi hiyo ni Tauhida Ramadhan Abdalla ambae alifungua kesi dhidi ya Ali Ali Ali madai yake katika kesi hiyo kwa mujibu wa hati ya madai ni kwamba Wadaawa ni wanandoa ambao walifunga ndoa tarehe 13.7.2018 na katika maisha yao ya ndoa wamebarikiwa kupata Watoto wawili. Mkata Rufaa katika hati hiyo ameeleza kuwa mahari yake yalikuwa ni kabati, kitanda, godoro, meza ya kujipambia (dressing

table), na kabati la kupambia vyombo (show case) lakini hili kabati la kupambia vyombo hakuwahi kupewa na lilibaki kuwa ni deni.

Mkata Rufaa alieza kuwa wamekuwa hawana tena maelewano katika ndoa yao na Mpinga Rufaa amekuwa akimtolea maneno machafu kumwambia kuwa analala na baba yake na kuwa anamuona kama mwanawe wa kumzaa. Vile vile alieleza kwamba Mpinga Rufaa ameshamuacha mara mbili kwa kumpa talaka za kutundika. Ya kwanza ni pale alipomwambia akitoka na akienda kwa shangazi yake itakuwa ni talaka yake na Mkata Rufaa alitoka na kwenda huko, na ya pili alipomwambia kuwa akiondoka na kumwachia mahari yake, yaani vitu itakuwa ni talaka yake na yeye akafanya hivyo. Katika madai hayo Mkata Rufaa alidai talaka yake, apewe matunzo ya watoto waliozaa na pia amaliziwe deni la mahari.

Mpinga Rufaa katika hati ya majibu ya madai alipinga madai yote hayo na kusema kwamba hakuwahi kumtolea Mkata Rufaa maneno hayo wala kumwacha Mkata Rufaa kwa kumtundikia talaka. Yeye hayupo tayari kumwacha kwa vile hakuna sababu za kisheria. Alieleza zaidi kuwa yeye anavyofahamu ni kuwa Mkata Rufaa ni mke wake na anachotaka ni kwa Mkata Rufaa kurudi nyumbani kwake. Kwa upande wa mahari alieleza kwamba yeye alitoa mahari ya Shilingi milioni mbili (TZS 2,000,000) kama ilivyo katika cheti cha ndoa na wala sio vyombo. Mpinga Rufaa aliiomba Mahkama imuamuru Mkata Rufaa arudi nyumbani kwake na waendelee kuishi katika ndoa yao.

Kadhi wa Wilaya baada ya kusikiliza kesi hiyo alitoa hukumu yake tarehe 29.07.2020 kama ifuatavyo:

1. Mahakama inaamua kuitengua ndoa ya Mdai na Mdaiwa kwa Fas-khi.
2. Mahkama inaamuru Mdai apewe talaka yake.
3. Mahkama inamuamuru Mdaiwa kutoa huduma kwa watoto aliozaa na Mdai.
4. Mahkama inalikataa dai la mahari na kutupilia mbali dai hili.
5. Gharama za kesi hii kila upande utabeba gharama zake.

Mpinga Rufaa hakuridhika na hukumu hiyo na hivyo kukata rufaa katika Mahakama ya Kadhi wa Rufaa. Kadhi wa Rufaa baada ya kusikiliza rufaa hiyo alitoa hukumu yake tarehe 16.4.2021 ambapo kutokana na upungufu aliouona katika usikilizwaji wa kesi alitengua hukumu ya Kadhi wa Wilaya na kuamuru kesi hiyo ikasikilizwe upya mbele ya Kadhi mwengine.

Mkata Rufaa hakuridhika na hukumu hiyo na kukata rufaa katika Mahakama hii. Amewasilisha hati yake ya rufaa ikiwa na sababu nne za rufaa kama ifuatavyo:

1. Kwamba Mhe. Kadhi wa Rufaa ambaye ni msomi wa dini ameteleza kisheria kwa kuamuru na kuagiza kuwa shauri alilia lirejeshwe na kusikilizwa upya katika Mahkama ya Wilaya na kupangiwa Kadhi mwengine.
2. Kwamba Mhe. Kadhi wa Rufaa ameshindwa kutoa sababu Madhubuti na za kisheria zilizomfanya alirejeshe jalada katika Mahkama ya awali wakati taratibu zote zilikamilika na hukumu kutolewa. Hoja aliyoitoa Mh. Kadhi wa Rufaa kwa kunukuu kanuni moja tu kutoka Mahkama ya Nigeria haikutosha kuwa ndio kigezo cha maamuzi yake.
3. Kwamba Mhe. Kadhi wa Rufaa hakuwa na sababu ya kulirejesha jalada kusikilizwa upya kwa sababu hakukuwa na mapungufu katika hatua za awali kwani wadaawa wote walikuwepo walijieleza bila kunyimwa uhuru na hatua zote za usikilizwaji kesi zilifuatwa.
4. Kwamba Mhe. Kadhi wa Rufaa amejipotosha katika amri ya kutaka kesi isikilizwe upya ambapo kunawanyima haki yao kisheria kwa kitendo hicho kinapelekea kupotezewa muda na kunaonesha ishara ya upendeleo wa wazi anaopewa Mpinga Rufaa, kwani ndoa huwa hailazimishwi kuwepo endapo ikitokea mmoja wao hana tena mapenzi na mwenzake.

Mahakama hii iliwasikiliza Wadaawa kuhusiana na rufaa hii. Kwa upande wa Mkata Rufaa alieleza kwamba hakuridhika na uamuzi wa Sheikh Daud kwa sababu uamuzi ulishatoka katika Mahkama ya Kadhi wa Wilaya kuwa apewe talaka yake. Aliendelea kusema kuwa Sheikh Daud kasema hakuona vielelezo kutoka kwake vya kudai talaka. Mpinga rufaa alimpa talaka mbili za matamshi ya kutundika na pia alimwambia akimpa vitu vyake vya mahari ndio itakuwa talaka yake. Hivyo, alieleza kuwa yeye alipoondoka nyumbani kwake alimkabidhi vitu vyake vyote na sasa anachotaka ni talaka yake.

Kwa upande wa Mpinga Rufaa yeye alieleza kuwa hakumwacha talaka mbili na hakuna ukweli kwenye hilo. Walikwenda ofisi ya Mufti na Mkata Rufaa akarejeshwa kwake lakini alikataa kurudi. Pia walikaa kikao cha sulhu lakini baba yake Mkata Rufaa alikataa mwanawe asirudi kwake. Baadae kesi ililetwa Mahkamani lakini alisisitiza kuwa hakumwacha na wala hatomwacha. Zaidi anasubiri maamuzi ya Mahkama.

Mkata Rufaa aliendelea kusisitiza kuwa yeye hatorudi na kusema anachofanya Mpinga Rufaa ni kumhangaisha na chuo.

Baada ya Mahakama kuisikiliza rufaa hii na kupitia mwenendo wa kesi wa Mahkama ya Wilaya na Mahkama ya Kadhi wa Rufaa. Mzozo uliopo mbele ya Mahkama hii ni kuhusiana na dai la talaka. Mkata Rufaa katika sababu zake nne amepiga maamuzi ya Kadhi wa Rufaa kuirejesha kesi hii kwenda kuanza upya mbele ya Kadhi mwengine.

Tukianza na suala hili ni kweli Kadhi wa Rufaa baada ya kupitia hukumu na mwenendo wa Mahkama ya Kadhi wa Wilaya alieleza kwamba aliona upungufu na hivyo kutaka kesi kuanza upya. Lakini kwa bahati mbaya Kadhi wa Rufaa hakuuainisha upungufu huo. Hata hivyo, Mahkama hii inakubaliana na Kadhi wa Rufaa kwamba ni kweli katika hukumu na mwenendo wa kesi kulikuwa na upungufu wa kiushahidi na upungufu wa kiutaratibu wa uendeshaji wa kesi. Madai yaliyoletwa mbele ya Kadhi wa Wilaya yalieegemea hoja tatu ambazo ni:

1. Je Mpinga Rufaa alimtolea maneno ya matusi Mkata rufaa na maneno hayo yana athari gani katika ndoa.
2. Je Mpinga Rufaa mara mbili alimtundikia talaka Mkata Rufaa, na hivyo kufanya Mpinga Rufaa awe ameachwa talaka mbili.
3. Je ni kitu gani kilitolewa kama mahari ya Mkata Rufaa.

Hoja zote tatu hazikuthibitishwa katika Mahkama ya Kadhi wa Wilaya. Hivyo, hapakuwa na Ushahidi. Pia hata katika uendeshaji wa kesi kulikuwa na upungufu. Kiutaratibu baada ya kupokea hati ya madai na majibu ya madai Kadhi wa Wilaya alitakiwa kuandaa hoja zinazobishaniwa jambo ambalo hakulifanya. Pili alitakiwa Mdai ndio aanze kutoa maelezo yake na aite mashahidi wake pamoja na kutoa vielelezo vyake, na baadae Mdaiwa atoe maelezo yake, aite mashahidi wake na kutoa vielelezo vyake. Utaratibu huu haukufuatwa sawa sawa.

Hivyo, Kadhi wa Rufaa alikuwa sahihi kutengua maamuzi hayo, lakini pia Kadhi wa Rufaa alikuwa na uwezo wa kuvaa viatu vya Kadhi wa Wilaya na kuanza kuchambua ushahidi ulioletwa Mahkamani na hata kuwataka Wadaawa kutoa maelezo ya ziada na kuleta mashahidi wengine ikiwa kuna haja ya kufanya hivyo.

Hii ndio njia muafaka hasa katika kesi hizi za ndoa ambapo maamuzi yake yanatakiwa kutolewa kwa haraka ili yasiweze kuleta athari kwa wanandoa na kwa jamii. Kesi hii ilifunguliwa tarehe 11.6.2020 na hivi sasa ni tarehe 21.7.2022 miaka miwili imeshapita na bado muafaka haujapatikana kuhusiana na ndoa ya wadaawa hawa. Hivyo, kuirejesha kwenda kuanza upya na kama itakatiwa rufaa tena ina maana mgogoro huu unaweza kuchukua miaka 4 hadi kutatuliwa. Huu ni muda mrefu hasa katika masuala ya ndoa, talaka na madai ya matunzo ya watoto. Hivyo, Mahkama hii inavaa viatu vya Kadhi wa Wilaya na kuupitia ushahidi uliotolewa.

Kuhusiana na hoja ya kwanza kwamba Mpinga Rufaa alimtolea maneno ya kashfa Mkata Rufaa suala hili halikuwa na ushahidi, Mkata Rufaa hakuleta hata shahidi mmoja aliyeweza kuthibitisha kwamba Mpinga Rufaa alitoa maneno hayo ya kashfa. Hivyo, hoja hii inakataliwa kwa sababu haikuwa na ushahidi.

Kuhusiana na hoja ya pili ambayo ni kuhusiana na kutundika talaka mara mbili kama ilivyodaiwa na Mkata Rufaa. Kumbukumbu za Mahkama zinaonyesha kwamba Mkata Rufaa alishindwa kuleta mashahidi kuthibitisha jambo hili. Nae Mpinga Rufaa alikataa kulifanya jambo hilo na alikubali kulishwa yamini. Mahkama ilimlisha kiapo na Mpinga Rufaa alikataa jambo hilo. Kwa kuwa alikubali kula kiapo kisheria ni kusema kwamba talaka ya kutundika haipo na Mkata Rufaa bado ni mke wa Mpinga Rufaa.

Kuhusiana na hoja ya tatu je mahari yaliyotelewa yalikuwa ni kitu gani. Mkata Rufaa amesema kuwa yeye amepewa vitu ambavyo ni kitanda, godoro, dressing table, na kabati, lakini bado anadai showcase. Kwa upande wa Mpinga Rufaa yeye anasema ametoa pesa Shilingi milioni mbili, na cheti cha ndoa kinaonyesha hivyo. Ni kweli cheti cha ndoa kinaonyesha kilichotelewa ni pesa shilingi milioni mbili. Lakini Mahkama ilimuuliza Mpinga Rufaa ikiwa aliwasilisha pesa nyumbani kwa Mkata Rufaa. Alisema hakuwasilisha pesa bali alifuatana na familia ya Mkata Rufaa na kupita madukani na familia ya Mkata Rufaa kuchagua vitu wanavyovitaka na baadae yeye alitoa pesa kuvinunua vitu hivyo. Hivyo, kwa maelezo hayo imethibiti kuwa mahari yalikuwa ni vitu (samani) na wala sio pesa, na ndio maana hata deni lililobaki ni la showcase na wala sio pesa.

Baada ya kuzipatia ufumbuzi hoja hizo tatu na kusema kwamba Mkata Rufaa bado ni mke wa Mpinga Rufaa, Mkata Rufaa aliieleza Mahkama kuwa yeye kwa hali yoyote hamtaki Mpinga Rufaa na yupo tayari kuinunua talaka kwa kurejesha mahari

aliyopokea. Mpinga Rufaa naye alikubali kupokea vitu hivyo na kumpa talaka Mkata Rufaa kwa vile amedhihirisha kwamba hayupo tayari kuishi na yeye.

Hivyo, Mahakama hii imeona kuwa Kadhi wa Wilaya alikosea kisheria kwa kuitengua ndoa ya Mkata Rufaa na Mpinga Rufaa kwa *Faskhi* wakati hilo halikuwa dai la Mkata Rufaa. Vilevile *Faskhi* ina sababu zake ambazo hazimo katika zilizotajwa katika sababu za msingi wa madai. Vile vile Kwa upande wa uamuzi wa Kadhi wa Rufaa Mahkama inaona haikuwa busara kuirejesha kuanza upya kesi hiyo.

Hivyo, Mahkama hii inaelekeza kuwa ikiwa mke hamtaki tena mumewe pamoja na njia za suluhu kugonga ukuta, basi itolewe talaka ya *khuluu* ili kumpa mke nafasi ya kutengana na mume yasiendelee madhara, kwani *khuluu* imetoa fursa hii hata kama mke hana sababu zozote za kudai talaka seuze ikiwa anazo zikiwemo za ugomvi usiokwisha. Vile vile Mahakama inaeleza kwamba sio sahihi kuelekea katika *Faskhi* kutokana na hoja zilizoelezwa hapo juu.

Hivyo, maamuzi ya Mahakama ya Kadhi wa Wilaya na Kadhi wa Rufaa yanatenguliwa na inampa haki Mkata Rufaa ya kupata talaka ya *khuluu* kwa vile hatua za sulhu zimeshafanyika na kugonga ukuta. Mahkama hii inamuelekeza Mpinga Rufaa kupokea mahari yake ambayo ni kitanda, godoro, kabati na dressing table ambavyo tayari vipo nyumbani kwake na ndio itakuwa *khuluu*. Mahakama ya Kadhi wa Wilaya nayo inaamriwa kumthibitishia Mkata Rufaa talaka yake ya khuluu. Pia Mpinga Rufaa anaamriwa atoe matunzo ya watoto kwa mujibu wa uwezo wake, na pia kila upande una haki ya kuwaona watoto hao.

Hii ni hukumu iliyotolewa na Mahkama hii.

(Imes.) Abdul-hakim A. Issa
Jaji

21/7/2022

(Imes.)	(Imes.)
Sk. Sameer Zulfikar	Sk. Saleh Hakim
(Imes.)	(Imes.)
Sk. Juma Fakih	Sk. Kani Mkanga

MAHKAMA

Hukumu hii imesomwa leo tarehe 21/7/2022 mbele ya mkata rufaa, mpinga rufaa hakuwepo.

(Imes.) Abdul-hakim A. Issa
Jaji

21/7/2022

Nathibitisha kwamba hii ni nakala halisi ya hukumu

……..

NAIBU MRAJIS

MAHKAMA KUU, ZANZIBAR